

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA KUMI NA MOJA

16 APRILI, 2019



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA KUMI NA MOJA – TAREHE 16 APRILI, 2019

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.



WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):

Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI JUU YA OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni wa Ofisi ya Makamu wa Rais

(Muungano na Mazingira) kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

III. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

88. MHESHIMIWA PASCHAL YOHANA HAONGA (MBOZI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Kuna Watumishi katika Halmashauri nyingi za Wilaya nchini walikuwa Wanachama wa PSPF wamestaafu zaidi ya mwaka mmoja na hawajalipwa fedha zao za kiinua mgongo (*pension*) na kwa sasa wanaishi maisha ya tabu na mateso makali:-

- (a) Je, ni lini sasa Serikali itawalipa Wastaafu hawa;
- (b) Inasemekana kwamba Serikali imetumia vibaya fedha za PSPF ikiwa ni pamoja na kuwakopesha kwa baadhi ya watu na Taasisi; Je, Serikali haioni kwamba hii inaweza kuwa sababu mojawapo ya kucheleweshwa mafao kwa Wastaafu;
- (c) Fedha za kiinua mgongo ni mali ya Mtumishi anayestaafu; Je, kwa nini Mifuko ya Pensheni isiwakopeshe Wastaafu

watarajiwa angalau 40% ya fedha hizo bila riba pale inapobakia miaka kumi (10) kabla ya kustaafu.

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

89. MHESHIMIWA BONNAH KAMOLI (SEGEREA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Wananchi wa Kata za Kinyerezi, Bonyokwa, Segerea Liwiti, Kipawa, Kimanga, Kisukulu na Tabata wamekuwa wakitumia fedha na muda mwingi kwenda kutafuta bidhaa na huduma katika masoko ya Buguruni na Kariakoo kutokana na kukosa huduma hizo katika maeneo yao:-

- (a) Je, kwa nini Serikali isijenge Soko kubwa katika eneo mbadala lililo katikati na linaloweza kufikiwa na Wananchi hao kwa wakati;
- (b) Je, kwa nini Soko la Kinyerezi lililozinduliwa na Mwenge mwaka 2017 lisifunguliwe ili kutoa huduma kwa Wananchi wanaozunguka Soko hilo na maeneo ya karibu.

OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):

90. MHESHIMIWA CAPT. ABBAS ALI HASSAN MWINYI (FUONI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-
Changamoto za Muungano wetu bado zipo licha ya Vikao vya Kamati za pamoja kati ya SMT na SMZ kukutana mara kwa mara:-

- (a) Je, ni changamoto zipi zilizopata ufumbuzi tangu Serikali ya Awamu ya Tano iingie madarakani;
- (b) Je, changamoto hizo ni ngapi.

91. MHESHIMIWA MBAROUK SALUM ALI (WETE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa elimu kwa Watanzania hususan kizazi kipya, kuhusu Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ili kutoa


uelewa wa pamoja na dhamira njema za Muungano huo.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

92. MHESHIMIWA JANETH MAURICE MASABURI (KUTEULIWA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:- Nchi za China na Singapore zimefanikiwa kwa kiwango kikubwa kwa kuwekeza kwenye ujenzi wa Vyuo vya Ufundi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutenga bajeti ya kutosha ili kuwekeza kwenye Vyuo vya Ufundi ambavyo vitasaidia Vijana wengi kupata ujuzi na kujiajiri.



WIZARA YA KILIMO:

93. MHESHIMIWA MARTIN ALEXANDER MSUHA (MBINGA VIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:- Hivi karibuni Serikali ilibadilisha mfumo wa ununuzi na uuzaji Kahawa kwamba ni lazima kupitia Vyama vya Ushirika vya Msingi:

Je, ni Vyama vingapi vya Msingi vya Ushirika (AMCOs) vimeundwa Wilayani Mbinga kufuatia kubadilishwa kwa mfumo huo.

**94. MHESHIMIWA CONCHESTA LEONCE
RWAMLAZA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:- Serikali ilikuwa na mradi wa kujenga masoko katika eneo la Nkwenda na Murongo katika Wilaya ya Kyerwa lakini Masoko hayo hayajakamilika na yametelekezwa:-

Je, Serikali ilikuwa na malengo gani kujenga masoko hayo.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

95. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (BLW):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Kumekuwa na kilio cha uchakavu wa Vituo vya Polisi kwa upande wa Unguja na Pemba:-

(a) Je, ni Vituo vingapi vipya vya Polisi vilivyojengwa kwa upande wa Unguja na Pemba;

(b) Je, Vituo hivyo vimejengwa na kampuni gani na ni vigezo gani vilivyoangaliwa katika ujenzi wa Vituo hivyo;

(c) Je, ni lini Mhe. Waziri, Naibu Waziri pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara watafuatana nami kwenda kuviona Vituo hivyo vilivyochakaa.

WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

96. MHESHIMIWA JACQUELINE NGONYANI MSONGOZI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Barabara ya Likuyufusi – Mkenda yenye urefu wa km 123 inayounganisha nchi mbili za Tanzania na Msumbiji bado haijaanza kujengwa kwa kiwango cha lami:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami.

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

**97. MHESHIMIWA JUMA OTHMAN HIJA
(TUMBATU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:- Thamani ya Shilingi ya Tanzania inaendelea kuporomoka kila siku, kuporomoka huko kunachangia kwa kiasi fulani ugumu wa maisha kwa Wananchi wa kawaida katika kupanga mipango yao ya kimaisha:-

Je, Serikali ina mikakati gani ya kudhibiti mporomoko huo.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS
(MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

**DODOMA
16 APRILI, 2019**

**S. KAGAIGAI
KATIBU WA BUNGE**